

SPACE SCOOP

Bringing news from across the Universe to kids all around the world



Kiwanda cha Kutengeneza Nyota Kinakufa



Kwa kipindi kirefu sasa ulimwengu umekuwa ni kiwanda kikubwa cha kutengeneza nyota, umeshatengeneza nyota nyingi zisizohesabika kutokana na gesi na mavumbi yanayoelea angani. Ingawa kwa sasa kiwanda hiki kikubwa kinaonyesha kuanza kufa!

Kutokana na kukusanya maada nyingi zilizozagaa, nyota changa zinaongezeka uzito- kama barafu inayobiringita kwenye theluji na baadae kuwa nyota kubwa sana. Wanaastronomia wamegundua kuwa hali hii haijitekezi kila mara. Ambapo kwa sasa nyota zinazaliwa chache sana, mara 30 ukilinganisha na dunia ilivyokuwa changal! Dalili inayoonyesha kwamba kiwanda kilichoshamiri cha nyota kimeanza kufa.

Wanaastronomia wamefanya ugunduzi huu kwa kuchunguza uzalishwaji wa nyota kwenye galaxi ambazo zipo katika umbali tofauti tofauti. Kwa kawaida mwanga huchukua muda kusafiri na kufika kwenye uso wa Dunia, hivyo wakati tunaangalia galaxi za mbali, tunaziangalia kama jinsi zilivyokuwa zikionekana pale zilipotoa mwanga kwa mara ya kwanza - miaka bilioni iliopita huko nyuma! Hii inamaanisha kuwa kwa kuangalia galaxi katika umbali tofauti tofauti, pia tunaangalia miaka tofauti tofauti. Wanaastronomia wanatumia telescope kama kifaa chenye nguvu cha kuangalia nyakati: wanaweza kuchukua picha za galaxi changa, wakati ni za muda mrefu sana.

Wanaastronomia wanatabiri kuwa namba ya jumla ya nyota zote zinazozaliwa itaongezeka kidogo sana, na baada ya hapo uzalishaji utasimama moja kwa moja! Kutokana na hayo inaonyesha kuwa karibu nyota zote zimeshazaliwa katika ulimwengu. Kwa mfano Jua ndilo litatoa joto kwa ajili yako, watoto wako, wajukuu wako, vitukuu wako na vizazi vijavyo.

COOL FACT

Nyota hujizalisha; zinatengenezwa kutokana na mavumbi, lakini pia hulipuka na kutoa mavumbi zinapokufa.



More information about EU-UNAWE
Space Scoop: www.eu-unawe.org/kids/